

# HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA

SHULE YA SEKONDARI MBUGA,  
S.L.P 150,  
MAHENGE/ULANGA.  
TAR.....

KUMB: NA.MBSS/S2SS0/ADM/JI/2021/01

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBUGA,WILAYA ULANGA ,MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021.

## 1.UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza (I) katika shule hii mwaka 2021,

Shule ya Sekondari Mbuga ipo umbali wa KM 58 toka Makao Makuu ya Wilaya ya Ulanga. Muhula wa kuanza masomo kwa Mwaka 2021 unaanza TAREHE 11/01/2021 ,Unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia TAREHE 11/01/2021 na Mwisho wa kuripoti ni TAREHE 22/01/2021

## 2.MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1.SARE ZA SHULE.

#### (A) WAVULANA

- Suruali Nyeusi ya Marinda(2) Pindo la Chini la Suruali Liwe na Upana Usiopungua Inchi 16 na Usiozidi Inchi 20
- Suruali Ya Kijani ya Marinda (2) Pindo ya Chini ya Suruali Liwe na Upana Usiopungua Inchi 16 na Usiozidi Ichi 20
- Shati Jeupe Mikono Mifupi(Tomato)
- Soksi Nyeupe Pea Mbili
- Fulana Ya Damu A Mzee
- Viatu Vyeusi Vya Kamba Vyenye Visigino Vifupi
- Tai Nyeusi

#### (B) WASICHANA

- Sketi Nyeusi( Ivuke Magoti)
- Sketi Ya Kijani(Ivuke Magoti)
- Soksi Nyeupe Pea Mbili
- Shati Jeupe
- Tai Nyeusi
- Fulana Damu ya Mzee
- Viatu Vyeusi vya Kamba vyenye Visigino Vifupi (Hijabu) Kwa Wanaovaa Hijabu.
- 

(C)Sare za Michezo Fulana na Bukta Nyekundu kwa Wavulana.Fulana na Traki ya Chini Nyekundu kwa Wasichana

2.2 Madaftari 11,Kalamu Kutosha,Mkebe na Kamusi ya Kiingereza

#### 2.3.vifaa vya usafi

Ndoo ndogo ya lita 10,fyekeo na Jembe atakuwa anakuja navyo vinapohitajika

### 3.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

#### a) sheria na kanuni za shule

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
2. Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni jambo la lazima
3. Kuwahi katika shughuli zote za shule na nyingine utakazo pewa
4. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
5. Kutunza usafi wa mwili mavazi na mazingira ya shule
6. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
8. Kutunza mali za shule na za umma

#### 3.1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZA SHULE AU KUSIMAMISHWA SHULE.


- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi cocaine, mirungi, kubeli nakadhalika
- d) Ubakaji
- e) Kupiga au kupigana
- f) Kuharibu kwa maksudi mali za umma
- g) Kudharau bendera ya taifa
- h) Kuo au kuolewa
- i) Kutoa mimba
- j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi

#### 4.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni
- b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule

Tafadhari soma kwa umakini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

Uongozi wa Shule ya Sekondari Mbuga unampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kujiunga na Shule hii, hivyo tunamkaribisha sana mwanao Mbuga Sekondari



D.H. Mwakyoma  
Mkuu wa shule

**MKUU WA SHULE**  
**SHULE YA SEKONDARI MBUGA**  
**S.L. P150 MAHENGE-ULANGA**